UENEZAJI WA VIRUSI VYA UKIMWI KUPITIA DAMU
Na Eleanor Turnbull

Virusi vya ukimwi vinapatikana kwenye damu na maji maji yoyote ya mwili.virusi hivi hupenya na kuingia kwa damu na kuumiza CD4 .CD4 hupatikana kwa damu na hutupatia kinga mwilini kutokana na magonjwa tofauti. virusi vya ukimwi humaliza nguvu hizi za CD4 na kwa sababu hii kinga huenda chini na kusababisha mwili isiwe na kinga ya kutosha kutokana na magonjwa na kwa hivyo kusababisha mtu kushikwa na ugonjwa wa ukimwi.

Virusi vya ukimwi haviishi kwa muda mrefu nje ya mwili ya binadamu kwa hivyo ili mtu aweze kupatwa na ugonjwa huu virusi hivi ni lazima zimwingie kwenye damu kwa kupitia damu au maji maji ya kimwili. Njia ya muhimu ya kupitisha virusi hivi ni kwa kufanya mapenzi bila kujikinga ,tutawaonyesha vile asilimia tano hadi kumi (5% - 10%) ya virusi vinapitishwa kwa njia ya damu.

Njia Jasiri Za Kueneza Virusi Vya Ukimwi

Walio katika hatari ya kupata virusi vya ukimwi kwa njia ya damu ni kama wale wanaotumia madawa ya kulevya kwa kutumia sindano, wanaokosa damu na wale wanaoongezwa damu. Utumiaji wa sindano unaleta asilimia tano(5%) ya virusi vya ukimwi na virusi huletwa wakati zaidi ya mtu moja anatumia sindano moja au kutumia sindano ambayo ime tumiwa na mtu ambaye ana virusi wakati wanapotumia madawa ya kulevya ama kupewa dawa hospitalini.

Mwongozo wa kidunia unasema kama sindano inatumia na zaidi ya mtu mmoja basi ni lazima kuchomwa au kuchemshwa kwa dakika ishirini.vyombo vyote ambavyo hutumiwa kutoboa ngozi kama wakati wa kujidunga sindano,kutahiriwa au kujichora vinapaswa kuchomwa kwa dakika ishirini.

Jumuiya ya kimataifa WHO imeanzisha mradi wa kupatia watu sindano ambazo hutumika mara moja na pia kufundisha watu kutumia sindano moja kwa mtu moja ili kuweza kuteremsha ueneaji wa ukimwi.

Kuongezwa damu au kutibiwa na damu ambayo ina virusi vya ukimwi pia huleta ugonjwa wa ukimwi. Pande mbali mbali za dunia hupima damu ambazo zimetolewa kusaidia wagonjwa ili kuhakikisha ni safi ,lakini nchi zingine hazina njia ya kupima bado.Pia watu ambao wana virusi vya ukimwi ama wanajishuku hawafaiwi kupeana damu kwani wanaweza eneza virusi hivi na hii inahakikisha

kwamba damu ni safi. watu wengi wameambukizwa virusi hivi bila kujua kwa njia ya kuongezwa damu na habari hii imeonyeshwa na nchi ya uchina.

Wana habari wameandika ripoti kwa gazeti moja ya Economist na kueleza ya kwamba mwaka wa elfu tisa na tisini (1990) serikali ili wapa moyo watu maskini kuuza damu zao. Lakini watu wengi hawaku toa damu kwani wanaamini ni vibaya kutoa damu na kwasababu hii hospitali zilibidi kuchanganisha damu za watu tofauti na kupatia watu waliohitaji damu ,hii ilikuwa ni hatari kwani watu hao hawakuwa wamepimwa hali yao ya ukimwi na zaidi ya elfu hamsini na tano waliambukizwa virusi vya ukimwi wakati mmoja , na baadaye zaidi ya watu laki moja na elfu thelathini na tatu kwenye eneo moja waliambukizwa na kwasababu hii serikali ika amua damu zote zipimwe na wale walioambukizwa wakapatiwa matibabu ya bure.

Njia Ambazo Hazina Hatari Kubwa Ya Kueneza Virusi Vya Ukimwi

Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kupata virusi kwa kujidunga na sindano au wembe ambayo ina virusi vya ukimwi lakini hii inaweza kuzuiwa kwa kumeza madawa baada ya kujikata.

Mtu ambaye anaishi na mtu aliye na virusi vya ukimwi ana faiwa kujikinga kutokana na damu au maji maji ya mwili, vidonda dugu na matapiko ya mtu mwenye virusi ,anafaiwa kujikinga kwa kufunika vidonda vyote na vitambaa safi,kuvaa karatasi ama glovu wakati ana mwosha mgonjwa na pia kuosha mikono kila wakati ana mguza mgonjwa.

Pia anafaiwa kuzuia kutumia wembe, mswaki ,sindano au makali yoyote ambayo yametumiwa na mtu mwenye virusi.

Virusi haipitishwi wakati watu wana busu kwani hakuna damu inayohusika, lakini kama mdomo iko na vidonda, sana sana wakati mtu ni mgonjwa sana basi virusi vinaweza kupita.

Pia kuna ripoti iliyo andikwa mwaka wa elfu moja tisaini na saba ambayo ilionesha virusi vinaweza kupitishwa wakati mtu mwenye virusi ana muuma mwenzake ambaye hana virusi na damu na kidonda kupatana lakini pia kuna ripoti zingine zinazoonesha watu wengine walio umwa hawakuambukizwa virusi na kuonyesha hii si njia hatari ya kueneza virusi.

Njia Za Kueneza Ukimwi Ambazo Ni Hadithi Tu Na Hazina Ukweli

Virusi vya ukimwi havipitishwi na mbu, utafiti umefanywa na umeonesha ya kwamba mbu hawaenezi virusi vya ukimwi hii ni kwasababu mbu hutumia mate na hakuna damu inayo tolewa kwa hivyo haienezi virusi vya ukimwi ,mbu hueneza ugonjwa kama malaria. Virusi pia hupatikana kwenye jasho ,machozi na mkojo lakini hakuna ripoti yeyote imeonyesha ugonjwa wa ukimwi unapitishwa na maji maji hii ya mwili.

Njia Za Kujikinga

Hii ripoti inaonyesha njia mtu mwenye afya ana weza kuambukizwa virusi vya ukimwi kwa njia ya damu ,na kitu cha maana kujua ni njia ya kujikinga na kuji chunga.

Damu zote za kusaidia wagonjwa zina faiwa kukaguliwa na kupimwa vizuri. Sindano na makali yote yanapaswa kutumiwa kwa uhakika na kutumiwa mara moja tu.Pia makali yote yanapaswa kuchomwa au kuchemshwa na kutupwa kwa visanduku mbali na watoto.

Jumuiya ya kimataifa WHO na majumuiya mengine yameenza mradi wa kupatia watu wanao tumia madawa ya kulevya sindano ambazo zinapaswa kutumika mara moja tu. Hii njia ina saidia kumaliza ukimwi kwa watu ambao hutumia madawa ya kulevya ya kujidunga,kufanya mapenzi bila kujikinga na umalaya kwani watu wengi wanao tumia madawa utumia ukahaba ili kupata pesa ya kununua madawa haya.

Mwishowe nitamaliza kwa kusema virusi kuenezwa kwa damu ni asilimia tano hadi kumi (5 – 10%) na kwa hivyo haipaswi kusahaulika au kutopewa maana.

Njia zote za kueneza virusi vya ukimwi vinapaswa kuangaliwa kwa uangalifu ili kuteremsha nambari ya watu wenye virusi vya ukimwi.

Njia zote za jamaa na tabia ambazo hueneza ugonjwa wa ukimwi kupitia damu zina faa kuangaliwa kwa uangalifu na kueleweka vizuri.

Control of Communicable Diseases Manual, 18th Edition.

Where There is No Doctor, a Village Health Care Handbook for Africa, Ed. Werner, D., Thuman, C., Maxwell, J. & Pearson, A. pp. 75

Blood Debts" in The Economist, January 20th-26th 2007.

United Nations

Control of Communicable Diseases Manual, 18th Edition. Heymann, D.L (2004).

Blood-to-blood transmission of HIV via bite. *Int Conf AIDS 1996 Jul 7-12; 11:179 (abstract no. Mo.D.1728)*

Liberti T, Lieb S, Scott R, Nolan J, Malecki J, Kalish M, Jaffe H; Department of Health and Rehabilitative Services (HRS) Office of Disease Intervention,

Misperceptions about HIV and Its Transmission. In: The Body- The complete HIV/AIDS resource. Centre for Disease Control and Prevention.

Control of Communicable Diseases Manual, 18th Edition. Heymann, D.L (2004).